

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



TAARIFA KWA MAWAKALA WA FORODHA NA WAAGIZAJI WA SHEHENA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuwajulisha mawakala wote wa Forodha na waagizaji wa shehena kutoka nje ya nchi, kuwa mfumo mpya wa malipo kwa njia ya kielektroniki unafanyika kwa kutumia namba maalumu kwa kila shehena hivyo basi mnasisitizwa kuzingatia yafuatayo wakati wa kujaza fomu za ukaguzi hapa nchini (DI Form) au kukabidhi cheti cha ukaguzi (CoC);

- 1) Kuhakikisha kwamba nyaraka sahihi za shehena na nyaraka zozote ambazo zitasaidia katika kukidhi matakwa ya kanuni za uondoshaji wa shehena husika zinaambatanishwa;
- 2) Kukabidhi nyaraka zote kwa afisa wa dawati la PVoC endapo shehena husika ina CoC na baadhi ya bidhaa hazikukaguliwa huko zilikutoka;
- 3) Kuhakikisha kwamba mwagizaji wa shehena mwenye msamaha anaambatanisha nakala ya barua ya msamaha wa PVoC iliyotolewa na TBS.
- 4) Kuandika barua ya ufafanuzi endapo mwagizaji ana maelezo ya ziada ambayo hayatoshi kujaza kwenye "DI Form"

Shirika linasisitiza kuzingatia maelezo haya kwani kukabidhi nyaraka zisizo sahihi kutasababisha kukuandika ankara isiyo sahihi na hivyo TBS haitakuwa tayari kufanya marekebisho au kufuta ankara husika kwenye mfumo wa kielektroniki.

imetolewa na;
Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
simu: +255(022) 2450206
hotline: +0800110827
barua pepe:
info@tbs.go.tz
Tovuti: www.tbs.go.tz